BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kumi – Tarehe 22 Mei, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa Mwaka 2018/2019.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa Mwaka 2018/2019.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

270. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Muyuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa wametabiri kipindi cha mwaka huu mvua zitakuwa kubwa na huenda zikaleta athari kwa wakaazi wa maeneo ya mabondeni, hivyo hadhari zichukuliwe mapema.

(a) Je, Serikali imeshajipanga kukabiliana na maafa yoyote yanayokadiriwa kutokea kutokana na mvua hizo.

(b) Je, kuna fedha na rasilimali za kutosha kukabiliana na maafa endapo yatatokea.

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

10. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Muyuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Mnamo mwezi wa Febuari, 2018 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein alifanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri na kuunda Wizara moja mpya.

Je, wananchi wategemee nini kutokana na mabadiliko hayo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

35. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na matukio mengi ya watu wazima kuwadhalilisha na kuwabaka kinamama na watoto wadogo wa kiume na wa kike hali ambayo imeleta hofu katika jamii.

(a) Kwa kuwa wahalifu hao wengi hupata adhabu ya kifungo, je, kuna maeneo maalum ambayo wahalifu hao huwekwa huko gerezani.

(b) Kama hakuna sehemu maalum, Serikali haioni kwamba kuwachanganya na watu wengine kunaweza kuwafanya kuendelea na tabia hiyo mbaya wakiwa kifungoni.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

44. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Muyuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Hivi karibuni Serikali imepitisha Sheria ya Kuanzisha Usimamizi wa Viwanda Vidogo Vidogo ikiwa ni muendelezo wa mpango wa kuifanya nchi yetu kuwa ya viwanda.

(a) Tokea kutungwa kwa Sheria hiyo kuna tija gani imepatikana mpaka sasa.

(b) Hatua gani zimefikiwa za kuimarisha ukuwaji wa viwanda nchini.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

107. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa maonesho ya wajasiriamali wa Kilimo huko Dole ambayo yalifana sana na ahadi ikatolewa na Serikali kuwa maonesho yale yangekuwa endelevu kwa kila siku za Jumamosi na Jumapili. Hata hivyo, ahadi hiyo inaonekana haijatekelezwa vizuri kwa wajasiriamali wale hawapati ushirikiano katika kuendeleza maonesho hayo kama walivyoahidiwa.

(a) Je, Wizara imeandaa utaratibu gani kuendeleza maonesho yale kama ilivyoahidiwa.

(b) Kusita kwa maonesho yale inajenga picha gani kwa wajasiriamali, je Wizara haioni kuwa inawavunja moyo.

(c) Je, Wizara inatoa tamko gani kwa wajasiriamali wale kuhusu kuendelea kwa maenesho yale kwa siku za Jumamosi na Jumapili.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

191. MHESHIMIWA ASHA ABDALLA MUSSA (Jimbo la Kiwengwa) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Wananchi wa Kitope wanampongeza Mhe. Rais kwa kuifanyia matengenezo barabara itokayo Kinduni hadi Kitope kwa kiwango cha lami, hata hivyo, matengenezo hayo yamefikia kijiji cha Kichungwani na lengo la matengenezo imaliziwe mpaka Kitope Kituo cha Afya ili kuwaondoshea wananchi usumbufu na wanafunzi wakati wa mvua.

(a) Je, ni sababu zipi zilizokwamisha barabara hiyo isimalizwe.

(b) Ni lini barabara hiyo itakamilika kutoka Kidimni hadi Kitope Kituo cha Afya.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

121. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Wanamichezo wa Zanzibar wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo uhaba wa vifaa vya kufanyia mazoezi na vifaa vya mashindano.

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kusaidia wanamichezo.

(b) Je, katika mashindano ya baiskeli ambayo yanafanyika Zanzibar kwa Kanda ya Afrika, Serikali imesaidia vipi.

(c) Je, Zanzibar ina michezo mingapi ya kushindana kimataifa na ina vikundi vingapi vya burudani vinavyojulikana na Baraza la Sanaa.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2018/2019.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2018/2019.

Zanzibar,
22 Mei, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.